MWENYE MUADHAM AMIN AL-RUDAINY

1918 – 2002

IMEANDIKWA NA

MUHAMMAD MUADHAM AMIN

SHARIFF MUADHAM AMIN (MWENYE MUADHAM)

Shariff Muadham ibnu Sayyid Ahmadil Amin kwa Maarufu anajulikana kama Mwenye Muadham Mwenye Amin alizaliwa Mji wa Patte, Lamu katika mwaka wa 1918. Alilelewa na wazazi wake wawili na akapata mafudisho ya awali ya dini kutoka kwa Babake yake Mzazi Mwenye Amin na baadhi ya Walimu wa Qur'ani huko mjini Patte.

Baada ya Mafundisho haya, Babake akaona kuna haja ya kupata mafundisho ya ilmu katika mji wa Lamu – khususa katika chuo cha Riyadha ambacho kilianza kutowa mafunzo kwa kila anayetake kupata Elimu. Hapo ndipo Babake Mwenye Amin akampeleka kwa Sayyid ahmad Badawy Ibnu Al Habib Swaleh Jamalullay (Mwenye Badawy). Akanza Masomo yake hapo na piya aksoma Kwa Mashekhe wengine wa Lamu akiwemo Sayyid Muhammad Assaggaf na Sayyid Abdallah Arrudainy.

Alikuwa ni Mwenye bidii katika masomo yake na akawa ni hodari katika ilmu ya ya Fiq-hi na Nahwu mpaka akawa huwafunza wanafunzi wenzake. Mwenye Ezi Mngu alimbariki na hifdhi nzuri na akahifadhi vitabu mbali mbali.

Mwenye Muadham alipata bahati kubwa kwa Shaikh Lake Mwenye Badawy na akampenda sana. Aliwahi kusafiri safari ya Hajj na sheikh lake na piya akamuozesha binti ya Ukhti yake Sayyida Fatma Binti Abdallah Al Beidh.

Baada ya kupowa ijaaza na Shaikh Lake Ahmad Badawy, Mwenye Muadham alianza kusomesha pale pale Riyadha – Lamu na katika aliowafundisha ni:

- Sayyid Alwi (Mzee Mwenye) Bin Sayyid Ahmad Badawy. Mzee Mwenye alijifakhiri sana kujifundisha somo la Nahwu na Balagha Kwa Mwenye Muadham
- Sayyid Hussein Bin Sayyid Ahmad Badawy (Swahibul Maqam wa Riyadha)

- Sayyid Alwi Bin Sayyid Muhammad Din (Ustadh Alwi Sharif Din)
- Sayyid Swaleh bin Sayyid Muhammad Sayyid Ali Badawy (Shaikh Bahassan)

Mwenye Muadham baadae kwa Amri ya Mzee Wake Mwenye Amin, alirudi Mji wa Patte na akapewa ukumbi katika nyumba ya babake asomeshe watu wa Patte. Alisomesha katika ukumbi hunu usiku na Mchana, wanaume kwa wanawake wakija wakati tofauti mbali mbali. Akianza darasa zake saa tisa za Usiku hadi alfajiri na baada ya swala ya alfajiri hadi Wakati wa Adhuhuri.

Mji wa Patte ulikuwa umegawanyika sehemu mbili kwa tabaka za kijamii. Kulikuwa na Jamii ya watu wanaojulikana kama "waungwana" na Tabaka ya jamii duni waliojulikana kama "watwana". Mwenye Muadham pamoja na Babake walijaribu kuondosha fikra hizi kwa kupitiya elimu na piya kuwa karibu na kuishi na watu wa jamii duni. Mwenye Muadham alifunguwa

milango kusomesha watu wa tabaka zote na wakapatikana walimu kama:

- Ustadh Muhammad Lali (alisomesha katika chuo chake – Patte)
- Ustadh Ali Abdallah (Madrasatul Fat-hi)
- Ustadh Muhammad Abbas (Madrastaul Fat-hi)
- Maalima Khadija Lali

Madrasatul Fat-hi ni moja katika matunda ya Mwenye Muadham baada ya kusomesha katika ukumbi wa babake. Aliasisi Madrassa hini baada ya kupata changmoto kwa baadhi ya wanamji wa Patte.

Katika Mji wa Patte, Mwenye Muadham piya aliasisi tarawehe ya kuswali kwa juzuu kila siku na piya akawa yuwatembeleya Wanawake majumbani na kuwasomesha ili kusudi ilimu ipatikane katika kila nyumba. Aliaminin kuwa Mwanamke ndiye Madrassa ya Kwanza katika Familiya na wanawake ndio wenye uwezo wa kuwakuza wanavyuoni.

Mwenye Muadham piya aliwahi kuandamana na shemeji yake Sharif Said Al Beidh kwenda sehemu za Aruwa – Uganda na akawahi Kusomesha huko kwa mda mfupi

Katika hali yake ya kimaisha, Mwenye Muadham alitegemeya sana jasho lake, alikuwa na Kitaru cha Ardhi aliyepewa na baba yake huko Patte akilima Muhogo, Ndizi aina mbali mbali, Mahindi, Matango na mengineyo.

Katika Maisha yake ya Uzeeni, Mwenye Muadham aliishi Mji wa Mombasa na kutumiya Maisha yake Msikiti wa Anisa akaweka vikao vya Ta'alim na akawahi kusomesha:

- Maalim Uthman (Imam na Hafidhul Qur'an – Msikiti Anisa)
- Sayyid Sharif Karama
- Ustadh Muhammad Muswtafa
- Ustadh Abubakar Abrar
- Ustadh Umar Abrar
- Ustadh Muhammad Shee Dumila

Aliuhuyisha Masjid Anisa na kukawa na watu wengi dhaifu wakilala Msikiti na kufanya usuhuba nao akawa awatukuwa kila pahali kwenye swadaqaat ili wapate maisha yao ya kila siku.

Mwenye Muadham ni mmoja alikuwa Mcha Mngu, Mfanyi Ibada akikithirisha zaidi kusima Qur'an. Yasemekana alikuwa aweza kukhitimisha Mswahafu kila siku. Katika hali yake ya uzeeni na ugonjwa wa Maguu, Mwenye Muadham alikijitahidi kwenda Msikitini na kuswali swala zake zote kwa Jamaa tena hali ya kuismama. Alionekana na Khushui ya hali ya juu katika swala zake.

Sharif Muadham aliuguwa kwa mda mfupi kama siku kumi na akafariki nyumbani kwake Mombasa kabla ya kuzama jua siku ya Juma Tatu tarekhe 26th August 2002 sawa na 18th Jumaadal Uwlaa 1423 Hijri na akazikwa Kikowani upande wa seif Halwa.

Twamuomba Mwene ezi Mngu Amrahamu na Amkunduliye Qabri Yake iwe rawdhatun min riyaadhil Jannat

Imeandikwa na Muhammad Muadham Amin